JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# MAGAZETINI WIKI HII

Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA. Simu: +255 26 2310021 Barua pepe: km@sheria.go.tz



*CHAIRMAN of the Legal Reform Commission of Tanzania, Retired Justice January Msoffe (right) hands over reports of research findings on primary courts mode of operation, national elections commission and political parties to the Constitutional and Legal Affairs Minister, Dr Damas Ndumbaro in Dodoma, yesterday. (Photo by Iddy Mwema)*

**Dailynews Page 4 13/04/2023**

CamScanner

# Tume ya Sheria yatoa ripoti za taarifa 730

Habel Chidawali na Mainda Mhando, Mwananchi

**Dodoma.** Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) imekabidhi ripoti mbili zenye taarifa 730 za tafiti ya mapitio katika sheria za uchaguzi na ya uendeshaji wa Mahakama za mwanzo.

Taarifa hiyo inapaswa kupelekwa bungeni ili iwasilishwe kwa umma na kutoa nafasi ya kujua kilichopendekezwa baada ya kuelezwa jana kuwa bado ni siri.

Taarifa hiyo imetolewa ikiwa ni mwaka mmoja tangu mbunge wa viti maalumu, Neema Rugangira atoe hoja binafsi bungeni Aprili mwaka jana, akiomba Bunge litunge sheria ya uchaguzi na vyama vya siasa ili kuwapa nafasi wanawake kugombea uongozi.

Hata hivyo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro amesema kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kilitoa mapendekezo ya mabadiliko ya sheria ya uchaguzi, hivyo limefanyiwa kazi.

Hivi karibuni, Ndumbaro alisema wizara imetenga bajeti ya Sh9 bilioni kwa ajili ya kupitia mchakato wa marekebisho ya sheria na mabadiliko ya Katiba, ambayo imekuwa kilio cha wadau kwa muda mrefu.

Akiwasilisha taarifa ya kikosi kazi, mwenyekiti wake, Profesa Rwekaza Mukandala alisema baada ya kazi ya miezi 10 ya kikosi hicho, walipendekeza mambo makubwa matatu ambayo ni mikutano ya hadhara, sheria ya uchaguzi na mapendekezo ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji wakiomba usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Jana, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Januari Msofe alisema utafiti huo umebaini changamoto ya kutokuwepo kwa sheria mahususi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Pia, alisema kikosi kazi kilipita mikoa 17 na kilibaini hakuna sheria mahususi ya utatuzi wa migogoro ya vyama vya siasa, kwa sababu iliyopo haijampa mamlaka msajili wa vyama vya siasa kutatua migogoro na kufanya migogoro hiyo idumu kwa muda mrefu.

Msofe alisema utafiti wao umebaini kutokuwepo kwa sheria mahususi ya uchaguzi wa ngazi ya vijiji, mitaa na vitongoji; pia chaguzi hizo zinaongozwa na kanuni zinazowekwa na Waziri wa Ofisi ya Rais Tamisemi.

> **"Tume imebaini kujitokeza kwa uchache kwa wapiga kura, hali inayosababishwa na baadhi ya viongozi kutotekeleza ahadi wanazozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni au hofu ya kutokea kwa vurugu eneo la kituo."**
>
> Jaji Msofe

"Tume imebaini kujitokeza kwa uchache kwa wapiga kura, hali inayosababishwa na baadhi ya viongozi kutotekeleza ahadi wanazozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni au hofu ya kutokea vurugu eneo la kituo.

Kingine Jaji aligusia kuwa wamebaini kutokuwepo vituo vya kupigia kura mbali na makazi ya watu na upungufu wa sheria mahsusi au mfumo unaowawezesha Watanzania wa nje ya nchi na vizuizini kujiandikisha na kupiga kura.

Hata hivyo, Jaji Msofe alisema wadau walitoa maoni yao juu ya uandikishaji wa wapigakura kwa njia ya kielektroniki hauwezi kusimamisha demokra
nchini, hivyo mfumo usi
mike kwa madai nchi h
jaendelea katika usala
wa taarifa za zoezi la u
dikishaji na upigaji kura.

Akipokea taarifa hi
Waziri Ndumbaro alise
kutokana na malalamiko
kutokuwepo kwa usawa
kijinsia ndani ya vyama v
siasa, huu ni muda sah
sheria hizo kufanyi
marekebisho.

Dk Ndumbaro alise
kilio cha wanawake kus
iriki katika uchaguzi sio c
leo, bali kilianza siku nyi
na ukweli ni kuwa naf
yao imekuwa finyu ku
kana na tamaduni na m
katika jamii.

Alisema taarifa ya ma
endekezo hayo inapelek
bungeni kwa ajili ya wa
kuchangia na kuanza k
mchakato wa mabadili
hayo.



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro (kushoto) akipokea mapendekezo ya mapitio ya sheria zinazosimamia mwene do wa utoaji haki na sheria zinazosimamia uchaguzi na vyama vya siasa kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Kusimamia Sheria, Jaji mstaafu Januari Msofe, katika hafla iliyofanyika Jijini Dodoma jana. **Picha na Mainda Mhando**



CamScanner



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro (kushoto) akipokea ripoti kuhusu mapitio ya sheria zinazosimamia uchaguzi na vyama vya siasa nchini na sheria zinazosimamia utoaji haki katika mahakama za mwanzo zilizowasilishwa na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, January Msoffe mkoani Dodoma jana. (Picha na Iddy Mwema).

# Rita yakusudia kufuta bodi 743 za wadhamini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umetoa siku 30 kwa taasisi na asasi 743 zijieleze kwa nini bodi za wadhamini wa taasisi hizo zisifutwe.

Rita imeleeza kuwa bodi hizo hazijatekeleza maelekezo ya kufanya marejeo ya katiba na kupeleka marejesho ya kila mwaka ya taasisi hizo kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Dar es Salaam na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Rita, Angela Anatory, wakala umefikia hatua hiyo kutekeleza takwa la kisheria.

"Hizo taasisi na asasi 743 ni orodha ya awali, uchambuzi wa taasisi zaidi unaendelea lengo ni kuhakikisha wadhamini wa taasisi zote wanatekeleza majukumu yao kikamilifu kwa mujibu wa sheria, katiba na maslahi mapana ya taifa," alisema Anatory.

Alisema Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura ya 318, toleo la 2002 kifungu 23(1)(d) kinatoa maelekezo ya taasisi zote nchini zilizosajiliwa na Rita kufanya marejeo kwa mujibu wa sheria hiyo.

Anatory alieleza kuwa bodi hizo zina jukumu la kuwasilisha marejesho kwa msimamizi mkuu wa wadhamini kila baada ya miezi 12 na kuwa kushindwa kutekeleza takwa hilo ni kwenda kinyume na sheria na hatua dhidi yao zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufuta bodi husika.

Aidha, alieleza kuwa msimamizi mkuu wa wadhamini alitoa agizo la kutekelezwa ndani ya miezi sita kuanzia Julai mwaka jana na kuzitaka bodi zote za wadhamini zifanye marejeo na kuboresha katiba zao kwa lengo la kuweka ibara inayoainisha chombo cha juu cha taasisi husika kwa taasisi za kidini.

Pia bodi hizo zilitakiwa kuweka ibara inayoelezea namna ya utatuzi wa migogoro unavyofanywa kwenye taasisi husika na kuweka ibara ya muda au ukomo wa wadhamini kukaa madarakani.



CamScanner



*MINSTER of Constitutional and Legal Affairs, Dr Damas Ndumbaro in consultations with the Minister of State in the Prime Minister's Office (Policy Coordination and Parliamentary Affairs) Jenita Mhagama in Parliament, Dodoma yesterday. (Photo by Iddy Mwema)*

# Tume yabaini upungufu sheria uchaguzi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TUME ya Kurekebisha Sheria Tanzania imewasilisha ripoti mbili za mapitio ya sheria kwa Waziri wa Katiba na Sheria ikiwamo ya uchaguzi wa vyama vya siasa huku ikibaini kasoro tisa ikiwamo wanawake kunyimwa nafasi kulinganisha na wanaume.

Ripoti ya pili ni ya utoaji haki katika mahakama za mwanzo.

Akiwasilisha ripoti hizo Mwenyekiti wa Tume hiyo Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Januari Msofe, alisema utafiti umebaini kuwa kutokuwapo kwa sheria mahususi ya uchaguzi wa ngazi ya vijiji, mitaa na vitongoji, hivyo uchaguzi kuongozwa na kanuni zinazowekwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI).

"Aidha tume pia imebaini kujitokeza kwa uchache kwa wapigakura hali inayosababishwa na baadhi ya viongozi kutotekeleza ahadi wanazozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni, hofu ya kutokea kwa vurugu eneo la kituo," alisema. Pia alisema, uwapo wa vituo vya kupigia kura mbali na makazi ya watu na kutokuwapo kwa sheria mahususi au mfumo unaowawezesha Watanzania walioko nje ya nchi na vizuizini kujiandikisha na kupiga kura.

Jaji Msofe alisema wadau wametoa maoni yao juu ya uandikishaji wa wapigakura njia ya kielektroniki kuwa hakuwezi kusimamisha demokrasia nchini, hivyo mfumo huo usitumike kwani nchi haijaendelea katika kuhakikisha usalama wa taarifa za uandikishaji na upigaji kura. Kadhalika, alisema wako wadau waliosema uchaguzi kwa njia ya kielektroniki uendelee kutumika kwa kuwa utaondoa udanganyifu na uboreshwe ili kuwapa nafasi watanzania wanaoishi nje ya nchi kushiriki upigaji kura, kuongeza ukweli na uwajibikaji katika upigaji kura.

Jaji Msofe pia alisema kutokana na wagombea kutakiwa kugharamia michango na matumizi yote wakati wa uchaguzi na sheria kukataza kupokea michango ya fedha au vifaa kutoka kwa wafadhili miezi mitatu kabla ya uchaguzi, wadau wameeleza kuwa sheria hiyo inawakandamiza.

Alisema utafiti umebaini uwapo wa sheria hiyo inawanyima fursa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama hivyo kutoshiriki kikamilifu zoezi la uchaguzi kwa kushindwa kufanya kampeni.

Msofe alizungumzia pia mapitio ya mfumo wa sheria katika mahakama za mwanzo kwamba katika hilo wamekusanya maoni katika mikoa saba.

Alisema katika hilo utafiti umebaini kwamba mahakama hizo zilianzishwa kwa ajili ya kushughulikia mashauri ya mwanzo pekee na si mengineyo,na wadau wameshauri iondolewe sheria ya kuweka baraza la wazee.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema jukumu kubwa la Waziri wa Katiba na Sheria ni kupokea taarifa ya ripoti hiyo huku akiipongeza tume hiyo kutekeleza maelekezo yaliyotolewa Aprili, mwaka jana, wakati wakiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Dk. Ndumbaro alisema ilitolewa hoja juu ya ushiriki finyu na mazingira magumu ya wanawake kushiriki katika mchakato wa siasa,ambapo kwa mahususi kabisa sheria ya uchaguzi ilionyeshewa vidole. Alisema vyama vya siasa pia vilinyooshewa kidole ndipo wizara ikatoa maelekezo kwa tume kulifanyia kazi suala hilo.

Alisema Mwanasheria Mkuu wa serikali alitoa maelekezo ya kupitia taratibu za utoaji haki katika mahakama za mwanzo, hivyo leo amepokea taarifa za maeneo hayo.



CamScanner